



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
OFISI YA MKUU WA MKOA
KIDATO CHA KWANZA
MUONGOZO WA USAHIHISHAJI
HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MSIMBO:

1. Alama 10@1

i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	ix	x
C	C	A	B	D	B	A	C	D	C

2. Alama 5@1

ORODHA A	i	ii	iii	iv	v
ORODHA B	F	C	A	E	B

SEHEMU B (Alama 70)

3. i) **Historia**- ni mfululizo wa matukio yaliyotokea katika jamii Fulani ama taifa kwa ujumla yenye athari kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni
ii. **Maadili**- ni miongozo inayotawala tabia na matendo ya mtu mmojammoja au jamii kwa ujumla
iii. **Rushwa**- ni kosa la kimaadili na jinai linalosababishwa na kufanya vitendo vilivyo kinyume na maadili hivyo kumnyima mtu mwingine haki yake na hata kuharibu rasilimali za taifa.
iv. **Zama za mawe** - ni kipindi cha kale kabisa katika maendeleo ya sayansi ya mwanadamu ambapo zana zilizotumika ziliundwa kwa mawe
v. **Urithi wa Asili**- ni utajiri wa rasilimali za asili na mazingira mfano Ardhi yenye rutuba
@ Alama 02 = Alama 10
4. milima mfano mlima Kilimanjaro ni kivutio cha watalii. Hutuwezesha kupata fedha za kigeni
ii) Ardhi. Hutumika kwa shughuli za kilimo na makazi
iii) Bahari. Hutumika kwa shughuli za uvuvi na usafiri
iv) Madini. Huleta mapato makubwa pale yanapo uzwa
v) Misitu. Hutupatia mbao na mazao mengine ya misitu kama vile dawa
vi) Gesi. Ni chanzo cha nishati

vii) Mbuga za wanyama. Ni kivutio cha watalii.

Dondoo tano tu@A lama 2=10

5. i) kujenga utu, heshima na uaminifu miongoni mwa watanzania
- ii) kukuza na kudumisha uzalendo
- iii) Kukuza maadili na utii wa sheria
- iv) Kuchambua maendeleo ya jamii kabla na baada ya ukoloni
- v) Kubainisha mila na desturi zilizojengwa na jamii za asili za tanzania ili kurithisha vizazi vya sasa na vijavyo
- vi)Kujenda moyo wa kuipenda, kuilinda na kuithamini nchi ya Tanzania
- vii) Kuelewa tunapotoka na tulipokua na kutafakari na tunapotaka kwenda kama taifa

dondoo 5tu @Alama 2=10

6. i) Biashara ya vyakula vya asili
- ii) Burudani
- iii) Tiba za asili
- iv) Maonesho ya sanaa
- v) Utalii wa kiutamaduni
- vi) Utafiti wa mambo ya kale

Dondoo 5 tu @Alama 2=10

7. i)Mahitaji ya kijamii. Mfano zana bora za kilimo
- ii) Uvumbuzi wa kijadi. Mfano aina mpya ya matibabu ya jadi
- iii) Biashara na ushirikiano . mfano teknolojia ya kufinyanga kwa kuzungusha duara la udongo
- iv)Elimu ya jadi mfano mafunzo ya kutunza mifugo na arithi
- v) Utaratibu Wa Kijamii
- vi) rasilimali za asili
- vii) Mazingira ya kijografia
- viii) mabadiliko ya kidemografia
- viii) Uhamiaji

Dondoo 5 tu @Alama 2=10

8. i) Kushuka kwa ubora wa huduma na viwango vya utendaji wa kazi
- ii) Kushuka kwa heshima na hadhi ya taasisi
- iii) Kushuka kwa tija na ufanisi wa taasisi
- iv) Kushuka kwa imani ya wananchi juu ya serikali yao
- v)Kukwama kwa miradi ya maendeleo
- vi)Kuongezeka kwa umaskini
- vii) Matumizi mabaya ya rasilimali za umma

Dondoo 5 tu@ Alama 2=10

9. i) Vifo na maafa kwa jamii za pwani
- ii) Kuharibu viwanda vya asili
- iii) Wizi wa rasilimali za Taifa

- iv) Kudumaa kwa uchumi wa asili na kuanzisha uchumi tegemezi
 - v) Kuharibu mila na desturi za asili ya watanzania
 - vi) Unyonyaji uliotokana na kutumikishwa kama wazalishaji malighafi mashambani
- Dondoo 5 tu @Alama 2=10**

SEHEMU C (ALAMA 15)

10. Utangulizi **Alama 1 ½**

Kiini cha swali/hoja **Alama 02 ½**

- mgawanyo wa koo kutokana na migogoro katika kabila
- uhaba wa ardhi
- shughuli za kibiashara
- shughuli za kibiashara
- kutafuta aridhi kwaajili ya malisho
- mabadiliko ya kijografia/ majanga
- kuoja na kuolewa/muingiliano na jamii nyingine

Hitimisho Alama 01